JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# HALMASHAURI YA JIJI ARUSHA

*Unapojibu tafadhali taja:*

Kumb. Na. **ARD/22992/5**

**Tar:05 /03/2024**

Mkurugenzi Mtendaji,
Kituo cha uwekezaji(TIC),
S.L.P 938,
**DAR-ES-SALAAM.**

**YAH: KIWANJA NAMBA 1165 NA 1166 KITALU A BURKA KILICHOKO KATIKA HALMASHAURI YA JIJI LA ARUSHA.**

Rejea kichwa cha habari hapo juu,

2. Ofisi inapenda kukufahamisha kwamba kumbukumbu zilizopo zinaonesha hadhi ya umiliki wa viwanja hivi ni kwamba viwanja hivi vimepangwa katika Mchorowa Mipango Na. **05/ARU/CC/38/072023** wa tarehe 04.09.2023 na kupimwa na kusajiliwa katika ramani ya upimaji na. **187419** ambapo kiwanja namba 1165 kina ukubwa wa mita za mraba **2027** na kiwanja namba 1166 kikiwa na ukubwa wa mita za mraba **2300** vyote vikiwa na matumizi ya makazi.

3. Kwa mujibu wa kumbukumbu zilizopo zinaonyesha kwamba viwanja hivi vinatokana na mmiliki wa awali **DEEP WATER LIMITED** ambaye amefanya urejeshaji wa Kiwanja Na. 175/86/2 na kufanya upimaji upya.

4. Baada ya upimaji kukamilika mmiliki huyu wa awali aliviuza viwanja tajwa kwa kampuni ya **MIMO PROPERTY HOLDING LIMITED** ambao wamewasilisha maombi ya kumilikishwa .Hata hivyo baada ya kupitia nyaraka za usajili wa kampuni hiyo tumebaini wanahisa wa kampuni hiyo ni raia wa nje hivyo umilikishaji wake unapitia kituo chako (TIC).

5. Kwa kuzingatia ufafanuzi huu napenda kukufahamisha kuwa Ardhi husika haina mgogoro wowote .Hivyoili tuweze kuendelea na hatua zaidi za umilikishaji wawekezaji hawa wanaletwa kwako ili waweze kusajiliwa na kupewa cheti cha uwekezaji. Baada ya hatua hiyo ndipo ardhi hii itatangazwa kwa ajili ya uwekezaji.

Makao Makuu, Mkurugenzi wa Jiji la Arusha,20 Barabara ya Boma, S. L. P 3013, 23101 ARUSHA, Simu: +255 27 2548072/2503494, Nukushi: +255 27 2545768, Barua Pepe: cd@arushacc.go.tz Tovuti: www.arushacc.go.tz

CamScanner

*Neema Ulomi*
**Kny: MKURUGENZI WA JIJI**
**ARUSHA.**

Nakala: Wakurugenzi
Mimo Property Holding Limited,
S.L.P 3190,
**DAR –E-SALAAM.**



CamScanner